



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**  
**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Baraza la chuo cha Utawala wa Umma (IPA) linatangaza nafasi za kazi za **Naibu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi** na **Naibu Mkuu wa Chuo - Utawala, Mipango na Fedha** kama ifuatavyo:-

**1. NAIBU MKUU WA CHUO - TAALUMA, UTAFITI NA USHAURI ELEKEZI**

***Sifa za Muombaji:***

- a) Awe amehitimu shahada ya Uzamivu (PhD) katika fani ya Ualimu, Utawala wa Umma, Sheria, Usimamzi wa Rasilimali Watu au fani yoyote inayolingana kutoka Taasisi inayotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- b) Awe na Uzoefu katika mambo ya Taaluma au Utawala kwa muda usiopungu miaka mitano (5).
- c) Awe na uadilifu wa hali ya juu.

**Majukumu ya Naibu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi, ni pamoja na:-**

- a) Kumshauri Mkuu wa Chuo juu ya mambo yote yanayohusiana na Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi.
- b) Kuwasilisha matokeo ya mitaani kwenye Kamati ya Taaluma na Baraza la Chuo.
- c) Kusimamia utekelezaji wa miongozo yote ya kitaaluma inayotolewa na Chuo na vyombo vyengine vya usimamizi.
- d) Kusimamia na kuwa kiungo wa Idara zilizo chini yake.
- e) Kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Baraza au Mkuu wa Chuo.

## **2. NAIBU MKUU WA CHUO - UTAWALA, MIPANGO NA FEDHA.**

### ***Sifa za Muombaji:***

- a) Awe amehitimu shahada Uzamivu (PhD) katika fani ya Utawala wa Umma, Usimamizi wa Rasilimali Watu au fani yoyote inayolingana kutoka Taasisi inayotambulika na Serikali.
- b) Awe na Uadilifu wa hali ya juu.

### **Majukumu ya Naibu Mkuu wa Chuo - Utawala, Mipango na Fedha.**

- a) Kuwa Msaidizi na Mshauri Mkuu wa Mkuu wa Chuo katika mambo yote yanayohusiana na Utawala, Mipango na Fedha.
- b) Kusimamia mpango mkakati wa Chuo pamoja na miongozo yote inayotolewa na Chuo.
- c) Kusimamia na kuwa kiungo wa Idara zilizo chini yake.
- d) Kusimamia mambo yote yanayohusiana na utawala, mipango na fedha kama itakavyoelekezwa na Baraza au Mkuu wa Chuo
- e) Kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Baraza au Mkuu wa Chuo.

### **NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI:**

Barua za maombi ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili au lugha ya Kiingereza, zioneshe nafasi ya kazi inayoombwa na ziambatanishwe na mambo yafuatayo:

- a) Wasifu binafsi wa muombaji (CV).
- b) Vivuli vya vyeti vyenye ithibati (Certified Copies) vya kumalizia masomo pamoja na matokeo.
- c) Cheti cha Ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), kwa wale waliosoma nje ya Tanzania.
- d) Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa kilicho thibitishwa (Certified copy)
- e) Majina matatu ya Wadhamini, taarifa zao za mawasiliano na ripoti za muombaji (referee letters) zilizofungwa vizuri kwa usiri.
- f) Picha tatu za (passport size) zilizopigwa si zaidi ya wiki mbili zilizopita.
- g) Nambari ya simu na barua pepe (e-mail) ya muomabji.

- h) Vivuli vitatu vya kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi.
- i) Maombi yote yawasilishwe kwa Katibu Mkuu kwa kupitia anuani ifuatayo:

**KATIBU MKUU,**

**OR - KATIBA SHERIA UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**

**S. L.P 3356,**

**ZANZIBAR**

- a) Maombi yawasilishwe kwa kupitia barua pepe [ipa.maombi@zanajira.go.tz](mailto:ipa.maombi@zanajira.go.tz)
- j) Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe **29 Juni, 2023.**

**TANBIHI:**

- b) Manaibu Wakuu wa Chuo watahika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na wanaweza kuteuliwa kwa kipindi chengine cha miaka mitatu (3) kwa mujibu wa Sheria ya Chuo.
- c) Muombaji ainishe nafasi ya Uongozi anayoiomba, vyenginevyo maombi yake hayatozingatiwa.
- d) Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora. [www.utumishismz.go.tz](http://www.utumishismz.go.tz) na tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini [www.zanajira.go.tz](http://www.zanajira.go.tz)
- e) Mawasiliano yatafanywa kwa wale tu watakaotimiza vigezo (shortlisted).

**AHSANTENI**